


Ubunifu wa Kiswidi wabertilisha sekta ya hoteli ulimwenguni

Kitu muhimu zaidi kwa hoteli yoyote kinapaswa kuwa kuwapa wateja wake hali nzuri zaidi ya malazi. Huduma hii hata hivyo lazima pia ijumuushe kitanda chenye starehe zaidi; ahadi ambayo, hadi sasa, imekuwa vigumu kutimiza kwa kuwa wageni wote wana mahitaji yao ya kipekee. Hali hii itabatilika sasa kwani kampuni ya YouBed ya Uswidi inazindua uvumbuzi wa kitanda kinachompa mtumiaji starehe ya kipekee. Pamoja na Business Sweden, Baraza la Biashara na Uwekezaji la Uswidi, YouBed sasa inazindua kote ulimwenguni, kwa kupeleka uvumbuzi wake wa kitanda cha kipekee katika hoteli ulimwenguni kote.



Kampuni ya Uswidi ya YouBed imevumbua njia ya kurekebisha uimara katika godoro za ubora wa juu wa springi mahususi bila kubertilisha viwango vya starehe ya kulala, kwa kutumia rimoti. Suluhisho hili la kitanda kinachofaa kila mtu linaweza kupatikana ulimwenguni kote kuitia dhana ya kipekee ya kulala ambayo inaaminika kuwa inabertilisha sekta ya hoteli, na kuwezesha hoteli hatimaye kutoa huduma stahiki kwa kila mteja: dhamana ya kitanda kinachokuhakikisha starehe ya kulala vizuri usiku.

– Ustarehe maalum ya kulala ndiyo ulikuwa umekosekana ambao hatimaye utawezesha hoteli kufikia uwezo wao kamili. Tunatumai kuwa wengi wataona hii kama fursa nzuri ya kuboresha huduma zao za hoteli na ushindani.

Sitashangaa ikiwa uvumbuzi wetu utaleta mabertiliko makubwa katika tasnia ya hoteli, na ni jukumu letu kukuza maendeleo haya kwa njia bora zaidi. Kwa hivyo imetuchukua miaka mingi kubuni dhana hii ya starehe ya kulala, wakati huo huo pia tukitengeneza miundombinu na uwezo wa kukidhi mahitaji ya kimataifa yanayotarajiwa, anasema Mattias Sörensen, Mkurugenzi Mtendaji na mwanzilishi wa YouBed.

Dhana ya Starehe ya Kulala ya YouBed sasa inazinduliwa ulimwenguni kote kwa ushirikiano wa kipekee na Business Sweden na idara zingine za serikali. Ofisi 44 mpya za YouBed - zilizo na uwezo wa kutoa usaidizi kwa kila soko la ulimwengu - tayari zinaanzisha mazungumzo na vikundi vya hoteli za kikanda zinazotarajiwa kuongoza uzinduzi wa kimaeneo kote ulimwenguni.

— YouBed iliamua hapo mapema kutumia miundo yetu ya usaidizi iliyopo, njia ya mkato kwa kampuni zinazoongoza kufikia haraka masoko ya kimataifa. Tulipojiunga mapema katika mchakato huu, tuliweza kubadilisha ushiriki wetu kulingana na uhusiano huu wa biashara wa muda mrefu. Tunajivunia sana kuwa sehemu ya uanzishaji wa kampuni mpya ya kimataifa ya Uswidi, na kuunga mkono uvumbuzi wao mahususi kwa uwezo unaostahili, anasema Fredrik Fexe, Makamu wa Rais Mtendaji, Mkuu wa Mikakati na Maendeleo ya Biashara katika Business Sweden.

YouBed inapatikana kwa sasa katika Hoteli zote za Mövenpick huko Ulaya, na pia katika First Hotels za Scandinavia na Hoteli za Scandic. Dhana ya starehe ya kulala ya YouBed mwanzo inapatikana tu kwa uzinduzi wa chapa ya kampuni ambayo ni pamoja na kila hoteli iliyo kwenye kikundi. www.youbed.com

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na:

Bi Vera Obare, Meneja wa Ofisi ya YouBed Eastern Africa Ofisi, EasternAfrica@youbedglobal.com, simu: +254742001350

Kuhusu YouBed

Kampuni ya Uswidi ya YouBed imevumbua na kusajilisha hataza njia mpya ya kubadilisha uimara wa godoro za ubora wa juu wa springi mahususi. Marekebisho haya hufanywa haraka na kwa urahisi kwa usaidizi wa kidhibiti cha mbali, na bila kuathiri viwango bora zaidi vya kitanda na starehe ya kulala. Unaweza pia kuboresha sehemu mbalimbali za godoro kivyake (mabega na viuno) kufikia ustarehe bora zaidi kwa watumiaji wote, licha ya urefu, uzani, umbo la mwili au mtindo uliopendelewa wa kulala. Matokeo yake ni kitanda cha kwanza ulimwenguni kilichobin afsishwa ambacho kinahakikisha starehe, na kufungua fursa kubwa na kukuza thamani katika sekta ambapo kulala na vitanda ni muhimu zaidi.

Kuhusu Business Sweden, Baraza la Biashara na Uwekezaji la Uswidi

Business Sweden, Baraza la Biashara na Uwekezaji la Uswidi, husaidia kampuni za Uswidi kuongeza mauzo yao ya kimataifa na kampuni za kimataifa kuwekeza na kupanuka nchini Uswidi. Business Sweden husaidia kampuni za Uswidi kwa kufupisha wakati wa mauzo, kupata vyano vipya vya mapato na kupunguza hatari. Pia husaidia kampuni za kimataifa kupata fursa mpya za kibashara, kuongeza faida kwa mtaji na kusaidia bila kubagua. Ikiwa na mtandoa katika viwango vyote, inatoa ushauri wa kimkakati na usaidizi wazi katika masoko 44 ya kuvutia zaidi ulimwenguni. Business Sweden inamilikiwa kwa pamoja na serikali na jamii ya wafanyakibashara.



Kuhusu kampuni

Ilianzzishwa:	2012
Mapato/Matookeo:	Hakuna mauzo kwani kipindi cha uthibitisho wa dhana kilikamilika mnamo 2018 ili kuboresha hali kwa uzinduzi kote ulimwenguni.
Bodi ya wakurugenzi:	Mattias Sörensen, Mkurugenzi Mtendaji na mwanzilishi Stefan Hyltenfeldt; Mkurugenzi wa Kiufundi na mwanzilishi Lars Björklund; Mkuu wa IP na rais wa zamani katika Shirika la Hataza la Uswid; Olle Bergström: GPMO na Shughuli katika Telia
Idadi ya ofisi:	44
Wafanyakazi na shirika:	Takribani 250 (pamoja na washauri), kati yao 14 wamo katika Ofisi ya Makao Makuu huko Stockholm na waliosalia katika ofisi 44 za maeneo kote ulimwenguni.
Masoko:	Ulimwenguni
Idadi ya wamiliki:	109
Mtaji uliochangwa:	Euro Milioni 6

Uvumbuzi

- Kampuni ya Uswid ya YouBed imebuni na kupata hakimiliki ya njia mpya ya kubadilisha uimara wa godoro za ubora wa juu wa springi mahususi, huku ikidumisha viwango vya juu vya starehe ya kulala wakati wote.
- Unaweza kurekebisha kwa urahisi godoro lote au sehemu tofauti kufanya kazi kivyake ili kupata hali inayokufaa zaidi. Marekebisho haya hufanywa kwa urahisi kwa kutumia rimoti inayodhibiti godoro zima.
- YouBed inayoweza kurekebisha inategemea teknolojia mpya kabisa ya utako wa kitanda, ambayo inaruhusu daraja mbili za springi mahususi kufanya kazi kivyake katika kitanda chote, kuchukua uzito na umbo la mwili la mtumiaji vizuri zaidi.
- Mfumo wa springi mahususi unaweza kufinyika kwa urahisi au kuachiliwa kwa kutumia rimoti, ili kufanya godoro liwe imara zaidi au laini zaidi, huku ukidumisha kikamilifu viwango vya juu zaidi vya ustarehe wa kitanda. Unaweza pia kuboresha maeneo tofauti ya ustarehe wa kitanda, mabega na viuno, kufikia hali inayokufaa zaidi.
- Kidhibiti cha mkononi wakati wote kitaonyesha hali kamili ya uimara wa jumla, kumpa kila mtumiaji maelezo ya kipekee ya starehe kwa matumizi ya baadaye.
- Pasipo kujali urefu, uzani, umbo la mwili au nafasi ya kulala inayopendelewa, YouBed itashughulikia mahitaji ya kibinaksi ya kila mtumiaji.



Uthibitisho wa dhana

Kulingana na zaidi ya vitanda vya Youbed 2 000 vilivyouzwa, tumeweza kuchambua na kupima athari halisi ya kubadilisha kitanda cha kawaida na cha YouBed kilichotengenezwa mahususi kwa mtumiaji. Matokeo kutoka kwa tafiti anuwai ni mazuri sana, ingawa sio ya kushangaza sana, kwani yanaonyesha athari ya mauzo ya huduma ya msingi ya tasnia kwa mara ya kwanza.

- Uchunguzi mkubwa wa NPS ulionyesha kuwa idadi ya Wakuzaji (kiwango cha juu zaidi cha kuridhika kwa wateja) iliongezeka kwa 14%¹ wakati kitanda cha kawaida kinabdalishwa na YouBed (ambapo kawaida 3-5% inachukuliwa kuwa hali ya mafanikio kwa kuzingatia kuongezeka kwa kuridhika kwa wateja).
- Uaminifu wa wateja uliongezeka kwa kiasi kikubwa. Zaidi ya 80% waliolala kwenye chumba cha YouBed wanasema watachagua aina ile ile ya chumba katika ziara inayofuata, ikilinganishwa na chini ya 20% kwa aina zingine za vyumba.
- Utayari wa kulipa zaidi umeongezeka na kiwango cha wastani cha chumba kuongezeka kwa Euro 20² kwa kila siku.
- Biashara ya vyumba na hoteli iliongezeka sana kwa sababu ya uwezo wake mkubwa wa kuvutia wageni wapya kwenye hoteli.
- Kipindi cha kupata malipo ya uwekezaji wa YouBed ni kati ya miezi 3 hadi 6, kumaanisha kuwa uwekezaji huo hurejeshwa mara 2 hadi 4 kila mwaka wakati wa urefu wa maisha wa bidhaa hii (mara 16-32 baada ya miaka 8).
- Kila hoteli itaalikwa kujaribu na kutathmini dhana na athari zake kabla ya uamuzi wa ununuzi kufanywa.



¹ <https://www.loopon.com/blog/adjustable-beds-study>

² Wastani kutoka kwa mapato anuwai na tafiti za kuridhika kwa wateja kwa washirika wa uthibitisho wa dhana: Hoteli na Mikahawa ya Mövenpick, First Hotels na Hoteli za Scandic.